



MAHAFALI YA NANE, CHUO KIKUU CHA KIMATAIFA CHA KAMPALA NCHINI TANZANIA



04 ALHAMISI
DISEMBA, 2025



01: 30
ASUBUHI



**VIWANJA VYA
MAHAFALI**



- 01:30 – 02:00 ASUBUHI - Wahitimu kuingia kwenye uwanja wa Mahafali
- 02:00 – 02:30 ASUBUHI - Wageni waalikwa na wafanyakazi wa KIUT kuingia kwenye uwanja wa Mahafali
- 02:30 – 03:00 ASUBUHI - Mgeni rasmi na wajumbe wa Baraza la Chuo na Seneti pamoja na waheshimiwa wengine kukusanyika katika ofisi ya Makamu Mkuu wa Chuo
- 03:00 – 03:20 ASUBUHI - Maandamano ya kitaaluma kuelekea kwenye uwanja wa Mahafali
- 03:20 – 03:40 ASUBUHI - Wimbo wa Taifa, ukifuatiwa na wimbo wa Afrika ya Mashariki na Wimbo wa Chuo
- 03:40 – 03:45 ASUBUHI - Makamu Mkuu wa Chuo kumualika rasmi Mkuu wa Chuo kuunda mkusanyiko wa Mahafali ya Nane ya KIUT 2025
- 03:45 – 03:50 ASUBUHI - Mkuu wa Chuo kuunda mkusanyiko wa Mahafali ya Nane ya KIUT- 2025
- 03:50 – 03:55 ASUBUHI - Burudani
- 03:55 – 04:15 ASUBUHI - Makamu Mkuu wa Chuo kuwatambulisha wageni rasmi
- 04:15 – 04:25 ASUBUHI - Hotuba ya Makamu Mkuu wa Chuo
- 04:25 – 04:35 ASUBUHI - Hotuba ya Mwenyekiti wa Baraza la Chuo
- 04:35 – 04:45 ASUBUHI - Hotuba ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini
- 04:45 – 05:05 ASUBUHI - Hotuba ya Mkuu wa Chuo
- 05:05 – 05:15 ASUBUHI - Burudani
- 05:15 – 05:45 ASUBUHI - Utoaji wa Tuzo na Vyeti
- 05:45 – 07:15 MCHANA - Kutunuku Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili
- 07:15 – 07:20 MCHANA - Mkuu wa Chuo kuvunja rasmi Mahafali ya Nane ya KIUT
- 07:20 – 07:45 MCHANA - Wimbo wa Afrika Mashariki na Wimbo wa Taifa.
- 07:45 – 07:50 MCHANA - Maandamano ya kitaaluma kutoka kwenye uwanja wa Mahafali
- 07:50 – 08:20 MCHANA - Chakula cha mchana kwa ajili ya wageni waalikwa



PHILOSOPHY

KAMPALA INTERNATIONAL UNIVERSITY IN TANZANIA draws its academic inspiration from the existentialist or phenomenological, and the pragmatist philosophy of education. The two conceptual frameworks focus on individual existence and the uniqueness of the individual learner and view the purpose of education as fostering cognitive and practical skills that will enable the learner to survive in a constantly changing world. The University is always driven by this philosophy to ensure that the educational programmes it offers benefit the clientele through provision of pragmatic courses of study and emphasises the uniqueness of each individual learner.

VISION

The Vision of the University is to become a premier institution of international repute that prepares students for the world and an inclusive society.

MISSION

The Mission of the University is to respond to societal and educational needs by designing and delivering education guided principles and values of respect for society, economy and to provide and develop a supportive research environment in which scholars at every stage of their carrier can flourish.



CORE VALUES:

Excellence: Through teaching and research, individually and corporately, to continuously raise standards for excellence, and deliver services beyond expectations.

Team work: Foster and nurture the value of team work and sense of belonging, while at the same time have a passionate commitment to a shared vision so as to fulfill the objectives of KIUT.

Internationality: Pursue international curriculum content, a globally relevant learning and employability culture befitting the international community of students and staff drawn from various countries.

Integrity: Embrace integrity, and nurture the culture of professionalism, honesty and fairness both in the official and private arena.

Principles of equal opportunity employment:

KIUT is an equal opportunity employer. Equity and transparency are the principles that guide the relationship between the University and its staff. To that end, the University does not discriminate against any employee or applicant in any manner that violates the law that is with regard to race, color, religion, national origin, sex, age, marital status, sexual, orientation, disability, political affiliation, personal appearance, family responsibilities, matriculation or any other characteristic protected under state law. Each person is evaluated on the basis of personal skill and merit.



MHE. SAMIA SULUHU HASSAN
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



AL-HAJJ DR. HASSAN BASSAJJABALABA
MWENYEKITI, BODI YA WADHAMINI




PROF. PETER MSOLLA
KAIMU MKUU WA CHUO




PROFESSOR YUNUS MGAYA
MWENYEKITI, BARAZA LA CHUO




PROF. HONORATHA MICHAEL MUSHI
KAIMU MAKAMU MKUU WA CHUO



DR. EDWARD KAMYA
KAIMU NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO TAALUMA



PROF. MARTIN O'RIELLY
NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO - FEDHA NA UTAWALA



ASSOC. PROF. ABANIS TURYAHEBWA
NAIBU MAKAMU WA CHUO – UTAFITI, UBUNIFU, USHAURI
ELEKEZI NA UJASIRIAMALI



WIMBO WA TAIFA LA TANZANIA



Ubeti wa Kwanza

Mungu ibariki Afrika
Wabariki Viongozi wake
Hekima Umoja na Amani
Hizi ni ngao zetu
Afrika na watu wake
Ibariki Afrika
Ibariki Afrika
Tubariki watoto wa Afrika.

Ubeti wa Pili

Mungu ibariki Tanzania
Dumisha uhuru na Umoja
Wake kwa Waume na Watoto
Mungu, Ibariki
Tanzania na watu wake.
Ibariki Tanzania
Ibariki Tanzania
Tubariki watoto wa Tanzania.





WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI



Kiitikio

*Jumuiya Yetu sote tuilinde
Tuwajibike tuimarike
Umoja wetu ni nguzo yetu
Idumu Jumuiya yetu.*

Ubeti wa Kwanza

*Ee Mungu twaomba ulinde
Jumuiya Afrika Mashariki
Tuwezeshe kuishi kwa amani
Tutimize na malengo yetu.*

Ubeti wa Pili

*Uzalendo pia mshikamano
Viwe msingi wa Umoja wetu
Natulinde Uhuru na Amani
Mila zetu na desturi zetu.*

Ubeti wa Tatu

*Viwandani na hata mashambani
Tufanye kazi sote kwa makini
Tujitoe kwa hali na mali
Tuijenge Jumuiya bora.*





KIU ANTHEM



Verse I

*Kampala International University
You are the torch that lights our path
In you we see our future bright
And by you the Nation gaineth from services pure
The emblem that you chose states the message
Unique is gait and truly the giant
With such height no success is too high
With such a size no task is insurmountable
Equipped with knowledge down to earth
We go out of your gates with dignity
May your vision bright and knowledge so abound
Be manifested in us as we serve the globe.*

Verse II

*Kampala International University
Your gates to success truly wide
Your way of teaching so unique
Always striving to give the globe the best of the best
You pave the way for those seeking knowledge
You pave the way for those seeking success
The young and old alike benefitting
To you the age is not a barrier
Equipped with knowledge, down to earth
We go out of your gates with dignity
May your vision bright and knowledge so abound
Be manifested in us as we serve the globe.*



HOTUBA YA KAIMU MAKAMU MKUU WA CHUO, PROFESA HONORATHA MUSHI, KWENYE MAHAFALI YA NANE YA CHUO KIKUU CHA KIMATAIFA CHA KAMPALA NCHINI TANZANIA (KIUT)



- Mkuu wa Chuo, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla
- Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, Mh. Al-Haji Hassan Basajjabalaba
- Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Profesa Yunus Mgaya,
- Wajumbe wa Baraza la Chuo
- Manaibu Makamu Wakuu wa Chuo
- Wajumbe wa Seneti ya Chuo
- Wakuu wa Vitivo, Idara na Kurugenzi mbalimbali
- Viongozi wa Taasisi mbalimbali za Serikali
- Viongozi kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali
- Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa
- Wahadhiri na Wafanyakazi wote wa Chuo
- Wazazi na Walezi
- Wahitimu
- Wanafunzi wote mliopo Chuoni
- Majirani zetu
- Waandishi wa Habari
- Wageni waalikwa
- Mabibi na Mabwana

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

1. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote aliyotujalia hadi kufikia siku hii ya leo ambapo tunaadhimisha sherehe za mahafali ya Nane ya Chuo chetu.

Napenda pia kukushukuru wewe kwa kukubali kuja kujumuika nasi na kuwatumu astashahada, stashahada na shahada mbalimbali wahitimu wetu wa mwaka huu 2025.

Pamoja na hayo ningependa tuwakumbuke wapendwa wetu ambao wametutangulia mbele haki mwaka huu. Hao wote ni wapendwa wetu una watabakia katika kumbukumbu za miyo yetu.

Kwa heshima yao naomba tusimame kwa dakika moja katika kuwaomba ili waendelee kukaa mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

2. Pia naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Chuo chetu, Al-Haji Dkt. Hassan Basajjabalaba, pamoja na wajumbe wote wa bodi. Tunashukuru sana kwa heshima mliotupa siku ya leo kwa kuhudhuria katika mahafali haya, ambayo ni matunda ya juhudi za pamoja.

Tunawashukuru sana kwa uwekezaaji wa kuendeleza miundombinu ya Chuo na katika kuimarisha ustawi wa Chuo chetu katika kipindi cha masomo cha mwaka uliopita. Uwekezaji huu Mheshimiwa Mkuu wa Chuo ni mfano wa kuigwa siyo tu kwa Tanzania bali barani Afrika.

Napenda pia kuwakaribisha wageni wote: viongozi wa Serikali, Wanasiasa, viongozi wa dini mbalimbali, mabalizi, viongozi wa Taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali, wazazi, walezi, ndugu, jamaa na marafiki. Uwepo wenu unaonesha kuwa mafanikio ya elimu ni jukumu letu sote.



Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

3. Pongezi za dhati ziende kwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Profesa Yunus Mgaya, pamoja na Naibu wake, Profesa Muhammed Ngoma kwa kutuonesha uongozi thabiti, usimamizi bora na mwongozo ambao umekuwa chachu ya mafanikio ya chuo.

Tunawashukuru kwa ushirikiano wa karibu mnaoutoa kwa Menejimenti ya Chuo chetu. Tunazithamini sana jitihada zenu, na tutaendelea kufanya kazi kwa bidii chini ya mwongozo wenu ili kuifikisha KIUT katika hatua za juu zaidi. Kama kauli mbiu yetu inavyosema **"Exploring the Height"**

Natoa shukrani pia kwa Wajumbe wote wa Baraza la Chuo na Kamati zake kwa usimamizi wao makini, umahiri wa kitaaluma na mwongozo wao makini ambao umeunda msingi wa mipango endelevu ya Chuo.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

4. Kwa furaha kubwa naomba nikutaarifu kupitia hadhira hii kuhusu maendeleo makubwa katika miundombinu ya Chuo chetu: kumbi za kufundishia, maabara, vifaa vya kisasa, na ubora wa rasilimali watu tulio nao.

Katika kipindi hiki, tumeongeza maabara sita (6) mpya za kisayansi zilizokamilika na zinazosheheni vifaa vya kisasa. Vilevile chuo chetu kimeongeza maabara ya kompyuta 1 na kufanya chuo kuwa na jumla ya maabara 25. Hizi zitawawezesha wanafunzi wetu kupata uzoefu wa vitendo, kufanya tafiti, na kukuza ubunifu.

Aidha, tumeimarisha maktaba, rasilimali za kidijitali, na kumbi zenye vifaa vya kisasa vya kufundishia ili kujenga mazingira mazuri ya ufunzaji.

Hatua hizi zimefanyika kwa kuzingatia miongozo ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU). Tunawashukuru sana TCU kwa mwongozo wao endelevu katika kuhakikisha viwango vya elimu vinabaki kuwa vya hali ya juu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

5. Tunaishukuru kwa dhati Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia TCU, NACTVET, Bodi za mikopo na wafadhili wote kwa miongozo yao katika kipindi hiki. Pia tunamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake thabiti katika kuboresha mazingira ya uwekezaji, ambayo yamewapa Bodi ya Wadhamini uhakika wa kuendelea kuwekeza KIUT.

Juhudi za serikali katika elimu zimeongeza kwa kiasi kikubwa mahitaji ya elimu ya juu, na sisi kama KIUT tumejipanga kupanua uwezo wa kudahili wanafunzi ili kuiunga mkono dhamira hii njema.

6. Kwa mwaka wa masomo 2024/2025 tulifanikiwa kudahili idadi ya kutosha ya wanafunzi katika programu zote zinazotolewa na chuo. Tunamshukuru Mungu kwa mafanikio haya na tunaamini idadi itaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Mafanikio yetu yametokana na ushirikiano thabiti na vyuo vikuu washirika, wadau wa utafiti na machapisho, na hospitali mbalimbali kama Muhimbili, Mwananyamala, Amana, Mloganzila, Temeke, Tumbi, Shree Hindu Mandal, na nyeninezo pamoja na maboresho ya mitaala yetu.

Pia Tunatanguliza shukrani zetu kwa timu za Tafiti ambazo zimejihusisha katika nyanja mbalimbali kwa kushirikiana na Taasisi rafiki za kikanda na kwingineko. Hii inahusisha mashirika kutoka Afrika ya Kusini (Chuo Kikuu cha Cape Town), Kenya (KEMRI), Nigeria (Kano Independent Research Centre Trust), Uganda (Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala) na Taasisi ya Mapafu ya (Chuo Kikuu cha Makerere), Tanzania (Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Nchini Tanzania and NIMR), Norway (Chuo Kikuu cha Bergen).

Moja ya jitihada za ushirikiano ni Mradi wa Kuboresha Mifumo ya Uamuzi wa Matibabu ya kifua Kikuu kwa Watoto unaotekelezwa nchini



Tanzania na Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Nchini Tanzania (KIUT) na Taasisi ya Utafiti wa Ugonjwa ya Kifua Kikuu (NIMR), na nchini Uganda na Taasisi ya Mapafu ya Chuo Kikuu cha Makerere na katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Chuo Kikuu Katoliki cha Bukavu. Mradi huu unafadhiliwa na EDCTP.

Pia nataka kuitambua timu inayofanya kazi katika Mradi wa Kuendeleza uundaji wa Mifano ya Malaria Barani Afrika (**Advancing Malaria Modelling in Africa Project**) (2025-2029), ambao unalenga kuimarisha afya na uundaji wa Mifano ya magonjwa kwa ajili ya kufanya maamuzi ya afya ya umma. Timu ya mradi inajumuisha **Dr Bruno Mmbando na Dr Amani Moran, Prof Angwara Kiwara, Prof Abanis Tyryahemwa, Prof Esther Ngadaya na Ms Khadija Pori**. Huu mradi unayofadhiliwa na Wellcome Trust kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Nchini Tanzania (KIUT), Chuo Kikuu cha Mlima Kenya (Mount Kenya University) Kenya, Chuo Kikuu cha Nairobi (the University of Nairobi) (Kenya), Imperial College London na Chuo Kikuu cha Bergen (Norway).

Zaidi ya hayo ninaipongeza timu inayoongozwa na Dr Nicholas Mnyambwa ambaye kwa sasa yuko katika **African Postdoctoral Training Initiative (APTI) Fellowship unaoadhiliwa na NIH**.

Pia tunawatambua na kuwapongeza wafanyakazi wote ambao wameandika hadi kufikisha tafiti 35 na wanafunzi ambao wamefaniwa kuandika tafiti zinazofikia 15 kwa kipindi cha mwaka wa masomo 2024/2025.

Katika kuungana na jitihada na maono ya serikali ya kupanua program za sayansi katika ngazi ya vyuo vikuu, KIUT inafanya tathmini ili kuanzisha program mpya za kitaaluma pamoja na:

- Bachelor of Science in Anatomy
- Bachelor of Science in Microbiology
- Bachelor of Science in Microbiology and Taxonomy
- Bachelor of Science in Physiology
- Bachelor of Science in Biochemistry

Jitihada hizi zinaakisi muendelezo wa utayari wetu katika kukuza taaluma, ubora katika tafiti na maendeleoya taifa.

Baada ya maelezo haya, napenda kukuwasilishia, Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, orodha ya wahitimu wa leo.

- Jumla ya wahitimu: 1,484 (772 wanaume), (712 wanawake)
- Wenye Vyeti na Stashahada: 821(381 wanaume), (440 wanawake)
- Wenye Shahada za Kwanza: 641 (380 wanaume), (261 wanawake)
- Wenye Shahada za Uzamili: 22 (12 wanawume), (10 wanawake)

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

7. Tunatoa shukrani za dhiti kwa Mwekezaji wetu, Al-Haji Dkt. Hassan Basajjalaba kwa jitihada zake zinazokivezesha chuo chetu kuimarika siku hadi siku. Uwekezaji wa kiwango hiki unahitaji weledi wa juu, Subira ya juu na maono yaliyosheheni ubora uliotukuka. Wahitimu wetu wa leo ni uthibitisho wa ubora huo.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

8. Kwa kumalizia, nawapongeza sana wahitimu wote.

Mmeishi nasi kwa mwaka mmoja hadi mitano au zaidi. Mmewumilia changamoto mbalimbali lakini mjue kuwa changamoto katika maisha ni jambo la kawaida na linalowajenga. Kitu cha muhimu ni kuzikubali na kutafuta njia ya kuzitatua changamoto hizo.

Nawasihii:

- Kuwa wabunifu na kutumia maarifa mliyopata.
- Kufanya kazi za kujitolea kupata uzoefu.
- Kutochagua kazi au maeneo ya kufanya kazi, mradi ni halali na yenye staha.
- Kuendelea kujifunza na kuongeza elimu
- Kuwa mabalozi wema wa KIUT Nawatakiya mafanikio mema katika safari yenu ya maisha.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza Nawatakieni Maadhimisho Mema ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2026.

HOTUBA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA CHUO PROFESA YUNUS MGAYA KATIKA MAHAFAJI YA NANE YA CHUO KIKUU CHA KIMATAIFA CHA KAMPALA NCHINI TANZANIA (KIUT)



- Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Profesa Peter Msolla,
- Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, Mheshimiwa Al-Haji Dr. Hassan Basajjabalaba,
- Wajumbe wa Baraza la Chuo,
- Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Honoratha Mushi,
- Manaibu Makamu wa Chuo,
- Wakuu wa Vitivo, Idara na Kurugenzi mbalimbali,
- Viongozi wa Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali,
- Wawakilishi wa Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa,
- Wahadhiri na Wafanyakazi wote wa Chuo,
- Wahitimu, Wazazi na Walezi,
- Wageni waalikwa,
- Mabibi na Mabwana.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

1. Napenda kuchukua fursa hii adimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka nyingi anazoendelea kutujalia. Leo tunasherehekea mahafali ya nane ya Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Nchini Tanzania ambapo ni siku ya mafanikio, matumaini na mwanga kwa wahitimu wetu na Chuo chetu kwa ujumla.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mkuu wa Chuo kwa kuheshimu mwaliko wetu na kuungana nasi katika kuwatunuku wahitimu: astashahada, stashahada na shahada mbalimbali. Uwepo wako umelifanya tukio hili kuwa la ladha ya kipekee.

Nawakaribisha viongozi wote wa taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za kiserikali, wawakilishi wa taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa, wahitimu wote, wazazi, walezi na wageni wote mliopo hapa.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

2. Napenda kuishukuru Bodi ya Wadhamini wa KIUT kwa ushirikiano wao tangu nilipoteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia mafanikio makubwa.

Ninashukuru kwa ushirikiano mzuri na imara kutoka kwa wadau wote wa Chuo. Kupitia uongozi huu, tumefanya marejeo na kuidhinisha programu mpya za masomo, kuajiri wahadhiri wenye sifa za juu, na kuimarisha ushirikiano wa kimkakati uliokifanya Chuo kuimarika zaidi.

Baraza la Chuo limekuwa likifanya vikao kwa utulivu, ufanisi, na tija. Tumekuwa tukiuchukulia kwa uzito ushauri wa wadau mbalimbali na kuufanyia kazi kwa mafanikio.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

3. Ninaikumbusha hadhira hii kuwa lengo kuu la kuwekeza katika elimu - kimataifa na kitaifa ni kujengea jamii uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali kama wasemavyo wahenga "Elimu ni ufunguo wa maisha."

Kuanzisha na kuendesha chuo kama KIUT ni hatua muhimu katika kupambana na umasikini, ujinga, maradhi na katika kuimarisha maendeleo endelevu na umoja wa Afrika.



Napenda kuipongeza Bodi ya Wadhamini kwa kujitolea kwao katika kuwekeza kwenye sekta ya elimu nchini Tanzania. Jitihada hizi zinachangia sana katika mustakabali wa taifa letu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

4. Kuongoza chuo kikuu binafsi kinachotoa elimu ya sayansi na teknolojia si jambo dogo. Inahitaji rasilimali fedha, rasilimali watu na uongozi madhubuti unaofuata sera, sheria na kanuni za elimu ya juu.

Kwa sababu hiyo, najivunia kutoa pongezi kwa uongozi wa juu wa Chuo chetu chini ya Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, kwa ushirikiano na manaibu wake, wakuu wa vitivo, idara na kurugenzi mbalimbali, tumepiga hatua kubwa katika mwaka wa masomo 2024/2025.

Uongozi wa Chuo unaendelea kuonesha weledi, maono, na uadilifu. Baraza la Chuo limefarajika sana kwa mafanikio haya, na linaamini kuwa uongozi bora utaendelea kuleta matokeo chanya zaidi.

Natoa wito kwa jamii nzima ya KIUT na watazania wote kwa ujumla kuendelea kuziunga mkono juhudi za uongozi wa Chuo ili kwa pamoja tuijenge nchi yetu, jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na Afrika nzima kwa ujumla kupitia utoaji wa elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

5. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imesaidia kuiwezesha Tanzania kufikia uchumi wa kati. Mafanikio haya yanatokana na uongozi imara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Hata hivyo, kufanikisha dira hii kunahitaji wataalamu mahiri wenye uwezo wa kutekeleza mipango ya maendeleo. Kwa kutambua hilo, Baraza la Chuo limepitisha marekebisho ya mitaala na kuidhinisha ujiri wa wahadhiri wenye sifa za juu ili kuongeza uwezo wa KIUT katika kufundisha, kufanya utafiti na kutoa huduma kwa jamii.

Tunatoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake katika elimu ikiwemo utoaji wa mikopo ya elimu ya juu, ajira kwa wahitimu, na sera zinazoweza ukuaji wa vyuo vikuu.

Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Profesa Adolph Mkenda, Waziri wa Elimu, kwa uongozi wake mahiri. Tunawashukuru TCU, NACTVET na bodi nyingine za taaluma kwa miongozo yao thabiti.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

6. Nawapongeza wahitimu wetu kwa juhudi na nidhamu mizoonesha tangu muanze masomo. Nawashukuru wahadhiri wetu: Maprofesa, wakufunzi, wasaidizi na watumishi wote wa Chuo kwa kazi yao kubwa.

Pia tunatambua mchango wa taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali, vyuo rafiki na wadau wa elimu wanotuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu ya Chuo katika kufundisha, kufanya utafiti na kutoa huduma kwa jamii.

Nawapongeza viongozi wa Serikali ya Wanafunzi (KIUTSO) kwa kuendesha majukumu yao kiweledi, uadilifu na uwajibikaji. Hii ni ishara ya kuwa wanaandaliwa vyema kuwa viongozi wa siku za usoni.

Ndugu wahitimu, elimu ni nyenzo yenye nguvu inayowawezesha kukabiliana na changamoto za jamii na kuleta maendeleo. Kwa muktadha huu elimu yetu inawawezesha kuwa na maono ya juu kama Twiga – **“Exploring the height”**

Maarifa yenu yawe chachu ya mabadiliko.

Jiwekeeni malengo, jitambueni, na tumieni ujuzi wenu katika kuleta maendeleo kwa jamii.

Nawatakia mafanikio mema katika maisha yenu yajayo.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza Nawatakieni Maadhimisho Mema ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2026.



HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI YA WADHAMINI, AL-HAJI DK. HASSAN BASAJJABALABA, KATIKA MAHAFALI YA NANE YA CHUO KIKUU CHA KIMATAIFA CHA KAMPALA NCHINI TANZANIA (KIUT)



- Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Profesa Peter Msolla,
- Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Profesa,
- Wajumbe wa Baraza la Chuo,
- Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Honoratha Mushi,
- Manaibu Makamu wa Chuo,
- Wakuu wa Vitivo, Idara na Kurugenzi mbalimbali,
- Viongozi wa Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizo za Kiserikali,
- Wawakilishi wa Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa,
- Wahadhiri na Wafanyakazi wote wa Chuo,
- Wahitimu, Wazazi na Walezi,
- Wageni waalikwa,
- Mabibi na Mabwana

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

1. Ni heshima kubwa kwa jamii nzima ya Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala Nchini Tanzania (KIUT) kukukaribisha leo katika sherehe hizi za Mahafali ya Nane ya Chuo chetu. Kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kutoa shukrani zangu za dhambi kwa uwepo wako. Tunatambua majukumu mengi mazito uliyonayo, na kwa uamuzi wako wa kuungana nasi siku ya leo, umetubariki na kutupa hamasa kubwa sana.

Uwepo wako ni ishara ya kuendelea kutuunga mkono, kutupa mwongozo, na kuonesha dhamira yako kwa maendeleo ya elimu ya juu nchini. Unatupa Faraja, nguvu mpya, na uwezo wa kujiamini, tunapoadhimisha tukio hili muhimu katika maisha ya wahitimu wetu.

Kwa niaba ya Bodi ya Wadhamini, nakukaribisha kwa moyo mkunjufu kwenye tukio hili adhimu. Aidha napenda kutoa salamu maalum za ukaribisho kwa wageni wote waalikwa, wakubwa na wadogo, wazazi, walezi, wahadhiri, wafanyakazi na marafiki wa Chuo waliojumuka nasi leo.

Zaidi ya yote, naomba niwakaribishe kwa dhambi wahitimu wetu ambao ndiyo kiini na fahari ya siku ya leo. Leo ni siku ya kilele cha bidii, nidhamu, na ustahimilivu wenu. Sherehe hii ni yenu, na tunaheshimishwa kushuhudia mwanzo wa safari zenu mpya. Karibuni nyote.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

2. Napenda pia kuchukua fursa hii kulishukuru na kulipongeza Baraza la Chuo kwa kazi kubwa na bora linayoendelea kuifanya tangu lilipoanzishwa miaka minane iliyopita. Nawapongeza kwa dhambi wajumbe wa Baraza kwa weledi, ustahimilivu na dhamira yao ya kukisimamia Chuo chetu, licha ya changamoto mbalimbali za kiutendaji. Nimejulishwa kuwa vikao vyote vya Baraza vimefanyika kama ilivyopangwa, jambo linalodhihirisha umakini wao. Nawashukuru sana kwa hilo.

Kwa kuwa tukio hili hukutanisha uongozi na jumuiya nzima ya KIUT angalau mara moja kwa mwaka, napenda kuungana na wote kuwashukuru kwa namna ya pekee hasa Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Profesa Yunus Mgaya kwa uongozi wake mahiri, weledi, na mwongozo mzuri anaoupa Baraza.



Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

3. Bodi ya Wadhamini inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliowezesha tufikie hatua hii muhimu. Tunakushukuru wewe Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, kwa ushirikiano wako, mwongozo na ushauri wako endelevu. Tunashukuru Baraza la Chuo, Menejimenti na jamii yote ya KIUT kwa misingi ya amani, utulivu na ushirikiano. Hakika umoja huu ndiyo siri ya mafanikio yetu. Bodi inaona matarajio makubwa ya ukuaji na maendeleo zaidi ya Chuo chetu katika miaka ijayo. Mwenyezi Mungu aendelee kutubariki sote.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

4. Shukrani za pekee ziende kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali yake kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), pamoja na taasisi nyingine za Serikali na na zisizo za kiserikali kwa kutuamini na kutukabidhi jukumu jema la kuchangia katika ujenzi wa taifa kupitia utoaji wa elimu bora.

Tunashukuru kwa miongozo na usimamizi ambao umetuwezesha kuboresha huduma zetu. Tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali na taasisi binafsi, katika kufanya kazi kwa bidii, na kuboresha Chuo chetu kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya TCU kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

5. Napenda kukumbusha kuwa dhamira ya Bodi ya Wadhamini ni kuisaidia Serikali katika juhudi za kuzalisha rasilimali watu yenye ujuzi wa hali ya juu itakayoshiriki katika maendeleo ya taifa. Dhamira nyingine ni kutoa fursa za ajira rasmi au zisizo rasmi kwa vijana kwa kuwapa ujuzi na maarifa kwa vitendo yanayowezesha kutatua changamoto binafsi na za kijamii.

Aidha, Bodi inawekeza katika Chuo hiki ili kutatua changamoto za jamii na kuchochea maendeleo kupitia sera yetu ya uwajibikaji kwa jamii. Kwa namna nyingine, Chuo hiki ni zawadi kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Kupitia Mfuko wa Udhambi wa KIUT, Bodi inaendelea kuwawezesha wanafunzi wa Kitanania wenye uwezo wa kitaaluma kutoka familia zenye changamoto za kiuchumi. Udhambi huu unatolewa kwa asilimia 50 ya ada ya masomo kwa wanafunzi wanaokidhi vigezo. Kwa sasa, mpango huu unawahusu wanafunzi wa shahada na stashahada katika programu zisizo za afya. Kila wilaya ya Tanzania Bara na Zanzibar inapata nafasi ya kupendekeza majina ya wanaostahili kupata udhamini huo.

Ili kuhakikisha tunaendelea kuzalisha Wataalamu Kesho, Bodi ya Wadhamini inaendelea kutoa ufadhili wa Masomo kwa Wanafunzi wapya kwa programu za masomo zisizo za afya kwa Astashahada, Stashahada na Shahada Mbali Mbali.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

6. Mwaka huu, Baraza la Chuo limefanikiwa kuanzisha maabara sita mpya za sayansi kama sehemu ya jitihada za kuimarisha utoaji wa elimu. Maabara hizi zimewekewa vifaa vya kisasa vitakavyowezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuboresha ubora wa ufundishaji na utafiti. Ujenzi huu unaonesha dhamira ya Baraza katika kuboresha mazingira ya kujifunza na kukuza ubora wa elimu ya sayansi.

Uwekezaji mwingine mkubwa kwa sasa ni kukamilisha Hospitali ya kufundishia inayojengwa hapa Chuoni. Hospitali hii itatoa huduma kwa jamii inayotuzunguka na kuwa kituo cha mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wetu. Bodi imejipanga kuhakikisha ujenzi unakamilika ifikapo mwaka 2026 na kuanza kutoa huduma mara moja. Aidha Baraza la Chuo limeathamirika kuboresha miundombinu ya kujifunzia kama maabara, maktaba, viwanja vya michezo pamoja na hosteli.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

7. Kwa kumalizia, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa wahitimu wote wanaopokea astashahada, stashahada na shahada zao mbalimbali katika siku ya leo. Hatua hii ni ushahidi wa jitihada, nidhamu na ustahimilivu wao katika safari yao ya elimu.




Bodi ya Wadhamini inawapongeza pia wahadhiri na wafanyakazi wote wa Chuo kwa kujitolea kwao katika kuhakikisha ubora wa taaluma, ushauri, mwongozo na malezi waliowapa wahitimu hawa umechangia pakubwa katika kuleta mafanikio yao. Tunawashukuru wazazi na walezi kwa kujitolea, kuvumilia na kuwaunga mkono wahitimu wao.

Kutokana na mahafali haya ya leo nina imani kuwa huko muendako mtatumia maarifa na ujuzi mliopata ili kutimiza malengo yenu na kuchangia katika maendeleo ya jamii zenu. Huo ni msingi na fahari ya Chuo chetu kuandaa wahitimu wanaolijenga taifa.

Kwa niaba ya Bodi ya Wadhamini, ninawatakia kila la heri popote muendako.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza na Nawatakieni Maadhimisho Mema ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2026.





HOTUBA YA MKUU WA CHUO, MHESHIMIWA PROFESA PETER MSOLLA, KWENYE MAHAFAJI YA NANE YA CHUO KIKUU CHA KIMATAIFA CHA KAMPALA NCHINI TANZANIA (KIUT)



- Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini, Mheshimiwa Al-Haji Hassan Basajjabalaba
- Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Profesa Yunus Mgaya,
- Wajumbe wa Baraza la Chuo
- Manaibu Makamu Wakuu wa Chuo
- Wajumbe wa Seneti ya Chuo
- Wakuu wa Vitivo, Idara na Kurugenzi mbalimbali
- Viongozi wa Taasisi mbalimbali za Serikali
- Viongozi kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali
- Wawakilishi wa Mashirika mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa
- Wahadhiri na Wafanyakazi wote wa Chuo
- Wazazi na Walezi
- Wahitimu
- Wanafunzi wote mliopo Chuoni
- Majirani zetu
- Waandishi wa Habari
- Wageni waalikwa
- Mabibi na Mabwana

Ndugu Mwenyekiti

1. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai hadi kufikia siku ya leo.

2. Pia, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyekiti wa baraza la wadhamini, pamoja na uongozi wote wa Chuo hiki kwa kunialika ili nijumuike nanyi katika kusherehekea mahafali haya mahafali haya ya 8 ya Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala nchini Tanzania (KIUT).

Ndugu Mwenyekiti,

3. Aidha naichukua nafasi hii kuipongeza Bodi yako ya Wadhamini kwa kuendelea kuwekeza katika Chuo hiki. Kama tulivyosikia katika hotuba zilizopita kuwa Bodi ya wadhamini imeleta maendeleo makubwa katika miundombinu ya Chuo: kumbi za kufundishia, maabara, vifaa vya kisasa vya kufundishia, na ubora wa rasilimali watu. Ni ukweli usiopindika kuwa kuongezeka kwa maabara sita za kisayansi na maabara tano za sayansi ya kompyuta zitawawezesha wakufunzi kufundisha kwa umakini zaidi na pia kutawawezesha wanafunzi kupata uzoefu wa vitendo, kufanya tafiti, na kukuza ubunifu. Kuimarishwa kwa maktaba, rasilimali za kidijitali na mengineyo, kutakiwezesha Chuo hiki kufikia malengo yake tarajiwa ya kujenga mazingira wezeshi ya ufundishaji kufuatana na kauli mbiu yake ya **Exploring the Height**.

4. Pia, Napata furaha na faraja kubwa kwamba Bodi ya Wadhamini imeweka mipango na nia ya kukamilisha ujenzi wa hospitali yetu mahali hapa kufikia mwiso wa mwaka 2026. Hakika huu ni uwekezaji muhimu utakaowezesha wanafunzi wetu wa masomo ya afya na udaktari kupata mahali bora pa kujifunza kwa vitendo. Pia uwekezaji huu utatoa mchango mkubwa katika kuboresha afya za wakazi wa maeneo haya na maeneo jirani, ili kuleta ustawi wa shughuli za kiuchumi na kijamii na kuboresha taswira ya eneo hili kwa ujumla. Tunamwomba mwenyezi Mungu afanikishe adhma hii.

Ndugu Mwenyekiti,

5. Pia, naomba niungane na wajumbe waliotangulia kuendelea kumshukuru Mwenyekiti wa Baraza la



Chuo hiki Profesa Yunus Mgaya kwa kuendelea kuliongoza Baraza la Chuo chetu kwa weledi uliotukuka. Pamoja na hayo ninatoa pongezi kwa wajumbe wote wa Baraza la Chuo hiki kwa kuendelea kutoa huduma iliyotukuka. Naamini kuwa kutokana na weledi na uzoefu wa wajumbe wa Baraza katika taaluma na sekta ya elimu kwa ujumla, chuo chetu kitaendelea kunufaika na kufika mahali bora zaidi kitaifa na kimataifa.

Ndugu Mwenyekiti,

6. Natoa pongezi kwa jumuiya yote ya Chuo Kikuu cha KIUT kwa umoja wao, mshikamano na utulivu unaoongezeka siku hadi siku. sambamba na kuendelea kushirikiana na majirani na taasisi zote za Kiserikali na zisizo za Kiserikali katika kutimiza majukumu ya kila siku. Yote hayo yanastahili pongezi maana amani na utulivu ni msingi wa maendeleo.

Ndugu Mwenyekiti,

7. Kwa kupitia jukwaa hili ninaomba sisi sote tuungane katika kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kwamba Taifa letu linazidi kuimarika kielimu, kijamii na kiuchumi. Kupitia kauli mbiu yake ya "Kazi na Utu tusonge mbele" Mheshimiwa Rais ametukumbusha kwa maneno na matendo kwamba kazi ndio msingi wa maendeleo na hakuna haki bila wajibu.

8. Aidha, ninapenda kuishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa kazi kubwa wanayofanya kutusimamia na kutupatia miongozo ya mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba elimu na mafunzo tunayotoa vinakuwa bora kwa manufaa ya wahitimu wetu na jamii kwa ujumla.

9. Nawaalika wanajumuiya wa Chuo Kikuu cha KIUT pamoja na watanania wote kwa ujumla, tuzidi

kumwomba Mheshimiwa Rais wetu afya njema ili sisi na vizazi vijavyo tuendeleo kunufaika na matokeo mazuri ya kazi yake. Vile vile tuendeleo kuiunga mkono Wizara ya Elimu na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) katika kujenga taifa la kistaarabu kupitia elimu bora.

Ndugu Mwenyekiti,

10. Sasa, sina budi kusema walau maneno machache juu ya wahitimu wa siku ya leo. Kwana kabisa nawapongeza kwa hatua hii muhimu mliyoifikia hasa kwa kusoma kwa bidii na kuishi hapa Chuoni kwa hali ya utulivu na maelewano muda wote wa masomo yenu. Bila shaka haikuwa kazi rahisi, na pengine iliwalizimu kujinyima baadhi ya fursa ili muweze kuwekeza katika elimu hii mnayojivunia leo.

11. Hivyo basi, npenda kuwakumbusha kwamba kazi ya maendeleo katika uchumi wa nchi yoyote ile inategemea sana kuwekeza katika maarifa na ujuzi. Ni matumaini yangu kuwa kufaulu kwenu ni ushahidi kuwa mmepata maarifa na ujuzi katika fani mlizosomea. Jamii inatarajia ya kwamba sasa mna upeo wa hali ya juu katika kupambana na changamoto zinazokwamisha maendeleo. Kwa kuamini hivyo tunawatunuku Astashahada, Stashahada na Shahada mbalimbali. Lakini uthibitisho mkubwa wa maarifa na ujuzi wenu utatokana na utendaji wenu huko muendako. Kila mara katika utendaji wenu kumbukeni usemi unaosema : "Binadamu wote ni sawa" hivyo nendeni mkahudumu bila kuwabagua Watanzania kwa kutumia kigezo chochote kile.

12. Nawasihi sana mkawe mabalizi wazuri wa jumuiya ya Chuo Kikuu cha KIUT kwa kuwa waaminifu, waadilifu na kutokushiriki kwa namna yoyote ile katika matendo yoyote ya kifisadi ili kulipatia Taifa letu maendeleo.

Ndugu Mwenyekiti,

13. Mwisho kabisa, nawapongeza wote mlioshiriki katika kufanikisha masomo ya hao wote wanaohitimu siku ya leo. Pia nawashukuru wote waliohiriki katika kuyaandaa mahafali haya.



Ndugu Mwenyekiti,

14. Napenda kuwashukuru sana Wazazi, Walezi, Wafadhili na Taasisi zilizoweza kuwadhamini wahitimu hawa kwa hali na mali katika muda wote wa masomo yao hadi kufikia siku ya leo. Nawaomba waendeleo na moyo huo huo.
Ndugu Mwenyekiti,

15. Kwa maneno haya, sasa niko tayari kutunuku Astashahada, Stashahada na Shahada na kutoa zawadi kwa wale wote waliohitimu na kufanya vizuri katika masomo yao.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza Nawatakieni Maadhimisho Mema ya Krismasi na Mwaka Mpya wa 2026.







LIST OF ACADEMIC STAFF TOP MANAGEMENT




**ASSOC. PROF.
HONORATHA M. K. MUSHI**
AG. VICE CHANCELLOR



DR. KAMYA EDWARD
AG. DVC - ACADEMIC
AFFAIRS



PROF. MARTIN G. O'REILLY
DVC - FINANCE &
ADMINISTRATION



**ASSOC. PROF. ABANIS
TURYAHEBWA**
DVC - RICE

DEANS, REGISTRY & DIRECTORS

Assoc. Prof. Joseph F. Kahamba

Dean - Faculty of Medicine & Pharmaceutical
Sciences

Dr. Kassim Rashid Kiliza

Dean - Faculty of Computing, Management & Social
Sciences

Dr. Zaharah Kiggundu Zaharah

Dean - Faculty of Education & Legal Studies

Mildred Phares Kinyawa

Dean - Faculty of Allied Health Sciences

Prof. Asuquo Olaitan Ruth

Associate Dean, Biomedical Sciences - Faculty of
Medicine & Pharmaceutical Sciences

Dr. Ayoub R. Magimba

Assoc. Dean, Clinicals - Faculty of Medicine &
Pharmaceutical Sciences

Okoruwa Godwin

Assoc. Dean, Pharmacy - Faculty of Medicine &
Pharmaceutical Sciences

Thembo Moses

